

# JE, UTAJUAJE UKO NA MAFUA?

Homa ya Mafua huzuka kila mwaka kuwaambukiza watu wa South Dakota katika jimbo lote—iwe unaishi jijini au mashambani, popote unapofanya kazi, kokote unakoenda kufurahia maisha pamoja na familia. Lakini, utajuaje ikiwa umeipata?

## JE, DALILI ZA MAFUA NI GANI?



### JOTO KALI

Iwe unalo joto lililopanda mwilini au unashuhudia baridi kali isiyoelezeka, unaweza kuwa umepata mafua ya msimu.



### KIKHOZI

Uchungu usiotulia kooni au kikhozi kikali mara nyingi ni moja ya dalili za kawaida sana za maambukizi ya homa ya mafua katika majira haya ya mwaka.



### KUTIRIRIKA KAMASI PUANI

Kupiga chafya na kutiririka kamasi puan kunaweza kuwa ni dalili ya homa ya mafua—usikisie ya kwamba ni “baridi tu!”



### MAUMIVU

Maumivu ya kichwa na misuli yanayoonekana kutoondoka yanaweza kuwa ni dalili ya mapema kwamba una mafua.



### UCHOVU MWINGI

Kuchoka na uchovu usioweza kuelezeza kwa tabia zako za kulala unaweza kuletwa na kirusi cha mafua.



**Je, una wasiwasi kuhusu homa ya mafua?  
Pata chanjo!  
Tafuta jinsi ya kupata kituo cha chanjo  
katika FluBug.org.**



SOUTH DAKOTA  
DEPARTMENT OF  
**HEALTH**

Imefadhiliwa na South Dakota Department of Health